Sura hii inaeleza maono aliyoonyeshwa nabii Zekaria, kuhusu ujenzi wa hekalu la pili. Anaanza kwa kuonyeshwa na malaika kinara cha taa cha dhahabu, chenye taa saba juu yake. Ambacho pia kina mirija saba, inayotoka katika matawi ya mizeituni miwili inayohusika kuleta mafuta katika kinara hiyo.

Hivyo nabii Zekaria kuona maono hayo, alitamani kuelewa tafsiri yake ni nini. Tusome.

> *Zekaria 4:1 Na yule malaika aliyesema nami akanijia mara ya pili, akaniamsha, kama mtu aamshwavyo katika usingizi wake.*
>
> *2 Akaniuliza, Unaona nini? Nikasema, Nimeona, na tazama, kinara cha taa cha dhahabu tupu, nacho kinabakuli juu yake, na taa zake saba juu yake; tena iko mirija saba ya kuleta mafuta, kwa taa zote zilizo juu yake;*
>
> *3 na mizeituni miwili karibu yake, mmoja upande wa kuume walile bakuli, na mmoja upande wake wa kushoto. 4 Nami nikajibu, nikamwambia yule malaika aliyesema nami, nikasema, Ee Bwana wangu, vitu hivi ni nini?*

*5 Ndipo malaika aliyesema nami akajibu, akaniambia, Hujui vitu hivi ni nini? Nikasema, La, Bwana wangu.*

*6 Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala sikwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.*

*7 Nani wewe, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tambarare; naye atalileta lile jiwe lakuwekwa juu kabisa pamoja na vigelegele vya, Neema, neema, ilikalie.*

*8 Tena neno la Bwana likanijia, kusema,*

*9 Mikono yake Zerubabeli imeiweka misingi ya nyumba hii, na mikono yake ndiyo itakayoimaliza; nawe*

*utajua ya kuwa Bwana wa majeshi amenituma kwenu.*

*10 Maana ni nani aliyeidharau siku ya mambo madogo? Kwa kuwa watafurahi, nao wataiona timazi katika mkono wa Zerubabeli; naam, hizi saba ndizo macho ya Bwana; yapiga mbio huko na huko duniani mwote.*

*11 Ndipo nikajibu, nikamwambia, Ni nini mizeituni hii miwili*

> *iliyo upande wa kuume wa kinara cha taa kile na upande wake wa kushoto?*
>
> *12 Nami nikajibu mara ya pili, nikamwuliza, Ni nini haya matawi mawili ya mizeituni, ambayo kwa njia ya ile mifereji miwili ya dhahabu hutoa mafuta yao?*
>
> *13 Akanijibu, akasema, Hujui hivi ni nini? Nikasema, La, Bwana wangu.*
>
> *14 Ndipo akasema, Hivi ni hao wana wawili wa mafuta, wasimamao karibu na Bwana wa dunia yote.*

Tafsiri yake ni kuwa matawi yale mawili walimwakilisha Yoshua kuhani mkuu, na Zerubabeli liwawi wa Yuda. Hawa ndio wana wawili wa mafuta. Yoshua alisimama katika mambo yote yahusuyo dini na ibada na Zerubabeli katika mambo yote ya kiutawala,

Na ile mizeituni miwili iliwakilisha Neno la Mungu lililowajia wao, kuwaongoza na kuwatia nguvu. aidha kwa njia ya Torati au kwa Manabii. Maana yake ni kuwa Yoshua kama kuhani mkuu akiongozwa na Torati na Zerubabeli kama akida akiongozwa na

manabii waliopokea ujumbe kutoka kwa Mungu ili walisimamie kusudi lake. Na manabii ambao walihusika hapa kuwatia nguvu walikuwa ni Hagai na Zekaria.

Katika ono hili Mungu alikuwa anamfunulia Zerubabeli uweza wake, kwamba si yeye atendaye hiyo kazi kubwa ambayo inaonekana kibinadamu haiwezekani, kutokana na hofu ya maadui zao, kupungukiwa fedha, na lile agizo lililotolewa na mfalme kuwa mji ule usiendelezwe. Bali ni Roho wa Mungu atendaye kazi yote, kwasababu si kwa uweza wao wala kwa nguvu.

Mungu akamuhakikishia Zerubabeli kuwa mikono yake ndiyo imetia msingi, na mikono yake ndiyo itakayoimaliza nyumba ile yote. Akimwonyesha kimaono jinsi wao wanavyosimama tu kama matawi ndani ya mzeituni (Zerubabeli na Yoshua), ambayo yanapokea mafuta na kutoa kuelekea kwenye mirija. Lakini hayahusiki katika kutengeneza mafuta au  kuwasha taa yoyote.

Na ndivyo ilivyokuwa kwao ujenzi huo ulienda ukakamilika bila taabu zao wenyewe walizozitarajia, bali Mungu alihakikisha anawapatia kibali, pamoja na vitendeakazi vyote(Mali) kiasi kwamba utukufu wa hekalu hilo la pili ukawa mkubwa sana kuliko

ule wa kwanza, pamoja na udhaifu wao.

Vivyo hivyo hata sasa, ni lazima tufahamu kuwa jambo lolote kuu tunalotamani kumfanyia Mungu, aidha kujenga nyumba yake, kusapoti injili, kuhubiri injili sehemu za taabu na nguvu n.k. Tusifirie sana hali zetu, bali tumfikirie Roho Mtakatifu, kwasababu yeye mwenyewe aliahidi kuwa atatupa nguvu ya kuyatenda hayo yote, na kuyatimiliza.(Matendo 1:8), ili utukufu wote umrudie yeye.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >> https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

> *Amka, Ee upanga, juu ya mchungaji wangu (Zekaria 13:7-9)*

> *DAMU YA ZAKARI BIN BARAKIA.*

> *Mafuta mabichi ni mafuta ya aina gani? (Zaburi 92:10)*

Rudi Nyumbani

Ile Mizeituni mwili na wale wana wawili wa mafuta vinawakilisha nini? (Zekaria 4)

Share on:
WhatsApp